



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**



Tarehe: 27/04/2023

Namba ya Kotesheni: LGA/071/2022/2023/RDC/W/36

**KWA AJILI YA UTOAJI WA HUDUMA YA UFUNDI WA UJENZI WA
MADARASA 2 NA MATUNDU 4 YA VYOO YA SHULE YA MSINGI KATUMBA
II KUPITIA PROGRAMU YA BOOST**

MWALIKO WA KOTESHENI

Kwa:

.....

.....

1. Serikali ya Tanzania imetenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa huduma ya Ujenzi wa Chumba kimoja cha darasa katika Shule ya Msingi **Katumba II** kupitia Programu ya BOOST kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Inakusudiwa kuwa sehemu ya fedha hizo zitatumika kugharamia malipo halali chini ya mkataba ambao unatolewa katika Mwaliko wa Kotesheni (MK).
2. Unakaribishwa kuwasilisha Kotesheni (Bei) kwa ajili ya utoaji huduma ya Ujenzi wa Miundo mbinu tajwa hapo juu kama ilivyoelekezwa kwenye Maelekezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika **Sehemu ya Pili. Miundo mbinu ya Shule hii inatarajiwa kujengwa katika shule ya Msingi Katumba II ni vyumba viwili vya madarasa na matundu 4 ya vyoo.**
3. Hivyo basi, wanahitajika mafundi ujenzi wenye sifa katika fani za Ufundi Uashi, Ufundi Seremala, Ufundi Aluminium na Ufundi Uchomeleaji (Grill)

- i. Fundi Uashi**
 - Awe na elimu ya ufundi Uashi/ujenzi na mwenye kujua kusoma ramani za majengo
 - Awe na mafundi wasaidizi wenye ujuzi wa kujenga, kusuka nondo kwenye rinta, usukaji wa mifumo ya umeme na kupiga rangi kwa unadhifu wa hali ya juu
 - ii. Fundi Aluminium**
 - Awe na uwezo wa kusoma michoro na vipimo vya ramani.
 - Awe na uwezo wa kutengeneza madirisha ya Aluminium na milango ya alco bond).
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.
 - iii. Fundi Seremala** (inahusisha utengenezaji wa milango na fremu za milango).
 - Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya mbao ngumu
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.
 - iv. Fundi kuchomelea vyuma** (ambao utajumuisha kutengeneza magrill ya milango na madirisha).
 - Awe na uwezo wa kutengeneza milango ya "grill"
 - Awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi katika majengo ya Serikali au kwenye makampuni.
- 4. Nyaraka za maelezo ya zabuni** kwa ajili ya mafundi kujaza kotesheni za ufundi husika zinapatikana katika ofisi ya **Mkuu wa Shule ya Msingi Katumba II, S.L.P 148, Tukuyu.**
- 5.** Kotesheni zote zilizojazwa kikamilifu kwa kuainisha Namba ya Kotesheni **LGA/071/2022/2023/RDC/W/35** zinatakiwa kuwasilishwa **Mkuu wa Shule ya Msingi Katumba II, S.L.P 148, Tukuyu**, yakiwa yamefungwa vizuri kwenye bahasha nyuma ya bahasha ikitaja jina la kazi inayoombwa na Shule husika na kitalu (Lot Na.) husika.
- 6.** Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni siku ya ijumaa ya Tarehe 04/05/2023 kabla ya saa 5:00 Asubuhi. Kisha baada ya muda mfupi Kotesheni zitafunguliwa kwa uwazi mbele ya Mafundi walioomba kazi tajwa hapo juu.
- 7.** Kotesheni ambazo hazitawasilishwa kabla ya muda uliotolewa hapo juu

hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini bila kujali mazingira yoyote yale.

8. Wako katika ujenzi wa Taifa.



Mchau, R.B

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE